**BODI YA KOROSHO TANZANIA**

# MAFUNZO YA UDHIBITI UBORA WA KOROSHO GHAFI MSIMU 2025/2026 KWA WADAU WA TASNIA YA KOROSHO NCHINI.

**Bodi ya Korosho Tanzania (CBT)** inapenda kuwataarifu wadau wote wa Tasnia ya Korosho nchini kwamba itaendesha mafunzo ya Uhakiki Ubora kuanzia tarehe **08/09/2025 hadi 12/09/2025** katika **Chuo cha Kilimo Mtwara (MATI)**. Mafunzo haya yanatolewa kwa mujibu wa kifungu namba 20(1) cha sheria namba 18 ya mwaka 2009 ya korosho na kanuni za mwaka 2010.

Mafunzo ya udhibiti ubora yatatolewa kwa watu wote wanaofanya kazi ama wenye nia ya kufanya kazi za uhakiki ubora katika msimu wa mauzo ya Korosho kwa mwaka 2025/2026. Mafunzo hayo yanalenga Wataalam wapya katika Tasnia ya korosho na wale wadau wote wa korosho ambao wanataka kujifunza kuhusu ubora wa korosho, wakiwemo wataalam wa Waendesha Ghala, Wanunuzi, Vyama vya Ushirika, Wamiliki wa Viwanda vya kubangua Korosho,Wataalam wa Ugani na Kilimo na Wadau wengine.

**Sifa za Mshiriki**:

- Mdau katika Tasnia ya Korosho mwenye nia ya kupata elimu ya udhibiti ubora wa korosho ghafi.
- Mtu mwenye elimu ya kilimo au taaluma zinazo shabihiana na kilimo atakuwa na sifa za kufanya kazi kwenye ghala za korosho nchini.

Gharama ya ushiriki wa mafunzo na kupatiwa cheti ni **Sh. 350,000/=.** Aidha, Wataalam kwenye ghala wenye vyeti vya miaka ya nyuma pamoja na Mameneja wa ghala zote nchini wanawajibika kuhudhuria bila kukosa siku ya tarehe **12/09/2025** kwa ajili ya kupata taratibu (*update)* za msimu 2025/2026 na mafunzo ya mfumo wa utoaji vibali vya kusafirishia korosho ghafi kwa gharama ya **Sh. 50,000/=** kwa kila mmoja. Malipo yote yatafanyika kwa kupitia namba ya malipo (Control number).

Kwa ajili ya kupata namba ya malipo na maelezo zaidi wasiliana na **Afisa Udhibiti Ubora CBT** ( **Eng. Jamal Akida**) kwa simu namba **+255 676 576 591**. Mwisho wa kupokea malipo ni tarehe **04/09/2025 saa 10:30 jioni**, baada ya kulipia hakikisha unatunza nakala yako ya malipo na kuja nayo siku ya mafunzo.

**Angalizo:**
Katika msimu wa mavuno 2025/2026, hakuna Mtaalam yoyote wa ubora atakayeruhusiwa kufanya kazi za uhakiki ubora wa korosho ghafi kwenye ghala za Minada, ghala za Wanunuzi na Viwanda vya kubangua korosho ghafi bila kuwa na cheti kutoka Bodi ya korosho.

Imetolewa na:

**MKURUGENZI MKUU**
**BODI YA KOROSHO TANZANIA**
JULAI 22, 2025.